BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAENDELEO YA WANAWAKE HABARI NA UTALII KUHUSIANA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE, WANAWAKE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma na Mwenye Kurehemu, kwa kutujaalia uhai na afya njema na tukaweza kukutana tena katika Baraza hili la Tisa kwenye Mkutano huu wa Kumi kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar.

Pia, nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Baraza kwa kuliongoza Baraza hili tukufu, naamini kwamba mtaliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu na kuimarisha Demokrasia katika muhimili huu muhimu wa dola katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuimarisha utoaji wa huduma mbali mbali za kijamii, kuimarisha miundombinu katika nyanja zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kutokana na hali hiyo, tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie afya njema, uadilifu, maarifa na hekima katika kuiongoza nchi yetu katika hali bora zaidi

Mheshimiwa Spika, Pia, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Mheshimiwa Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara hii.

Pia lakini pia nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kwa kiasi cha kunirahisishia kazi ya kuongoza kikao kuwa nyepesi, kwa hakika ni wajumbe mahiri wenye uweledi, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha kwa Wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Kwa heshima na taadhima napenda kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kama ifiatavyo:-

1.	Mheshimiwa Ali Suleiman Ali (SHIHATA)	Mwenyekiti
2.	Mheshimiwa Salha Mohammed Mwinjuma	Makamu Mwenyekiti
3.	Mheshimiwa Maryam Thani Juma	Mjumbe
4.	Mheshimiwa Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
5.	Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
6.	Mheshimiwa Mussa Foum Mussa	Mjumbe
7.	Ndugu Himid Haji Choko	Katibu
8.	Ndugu Mussa Issa Mussa	Katibu
9.	Ndugu Amina Abeid Hemedi	Mkalimani

Mheshimiwa Spika, Baada ya utangulizi huo mfupi, sasa naomba nichukue nafasi hii adhimu kutekeleza jukumu lililonileta hapa mbele ya Baraza lako tukufu moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ina fungu (*vote*) moja (1) ambalo ni Q01 na imepanga kutekeleza Programu Kuu tano zenye Programu Ndogo Kumi na Nne (14) ambapo kwa ujumla fedha zilizoombwa kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto ni **Tshs. 15,590,600,000 (Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Tano na Tisiini na Laki Sita).**

Programu Kuu ni hizi zifuatazo:-

1. Programu Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

2. Maendeleo ya Wanawake na Kupinga Udhalilishaji

3. Hifadhi ya Jamii na Maendeleo ya Wanawake na Watoto

4. Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto

5. Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu haikuridhika sana na mapato ya asilimia 69 yaliyokusanywa na wazara hii mwaka wa fedha 2017/2018, na kuomba wizara hii iongoze juhudi za ukusanyaji na kuibua zaidi viazio vipya vya mapato badala ya kutegemea ada ya malipo ya vibali vya kazi kwa wataalamu wa Kigeni kama ni kiazio kikuu cha mapato kwa wizara hii.
Lakini pia Kamati haikuridhika na Kasma waliyopangiwa kukusanya kwa Mwaka 2018/2019 ambayo ni Shilingi 794,613,000/= (***Milioni Mia Saba na Tisini na Nne, Laki Sita na Kumi na Tatu Elfu)*** kwa kuwa kiwango hiki ni kidogo kulinganisha na

cha mwaka unaomalizika, ambapo walikadiriwa kukusanya shilingi **855,000,000/=** (***Milioni Mia Nane na Hamsini na Tano).*** Kamati inawasiwasi ni kwanini Bajeti ya Wizara inakua inaongezeka kila mwaka na kukuza huduma za wizara lakini mapato ya wizara yanapunguzwa.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha kwamba kumekuwa na Mafanikio ya urejeshaji wa Mikopo wa wastani wa asilimia 96. Kamati inapongeza hatua hii na kuitaka Wizara isiridhike lakini iongeze juhudi za

Kamati, inatoa msisitizo kwa Wizara kwamba ihakikishe kuwa inaongeza bidii katika kuwafuatilia kwa karibu wananchi au wajasiriamali wanaowapa mikopo, ili kurejeshwa kwa wakati kwa lengo la kuwanufaisha wananchi (wajasiriamali) wengi.

Mheshimiwa Spika, Wajaasiriamali wetu wamekuwa wakijitahidi sana kuzalisha hasa kilimo cha matunda lakini wamekuwa wakivunjika moyo kutokana na tatizo sugu la ukosefu wa soko la bidhaa zao, linalosababishwa na kukosa mfumo na Viwango bora vya usindikaji na usarifu wa bidhaa zinazozalishwa na vikundi vyetu.

Aidha Bei kubwa ya pembejeo za Kilimo , hasa kilimo cha Maweni pamoja na taaluma ndogo kuhusiana na shughuli zao bado zinakwaza katika kutekeleza vyema majukumu yao Hivyo , Kamati inaishauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Biashara na Viwanda ili kuangalia uwezekano wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya usarifu wa mazao au kutafuta wawekezaji ama kuingia ubia ili kuyahami mazao ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu kwa mara nyengine tena inaishauri wizara na serikali kwa ujumla kuangalia uwezekano wa Kupunguza bei za Pembejeo kwa wakulima wa maweni ambao hivi sasa wako mstari wa mbele katika kilimo cha Ndimu, machungwa na tungule kilimo ambacho hivi sasa kinakubali vizuri katika maeneo mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati, inatoa pongezi za dhati kwa Wizara kwa namna ya ilivyoweza kutekeleza majukumu yake ya kuratibu shughuli za kijinsia. Hata hivyo, Kamati inaiunga mkono Wizara kwa kuendelea kupiga vita vitendo vya udhalilishaji wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, kwa furaha Kamati inapongeza hatua ya rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutia saini **Mswada wa Sheria ya Adhabu na Sheria ya Mwenendo wa Jinai** na kuwa Sheria Kamili. Kamati inaamini kwamba, Sheria hizo hivi sasa zitasaidia kupunguza wimbi la Vitendo vya udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto
Aidha, Kamati imefurahishwa na taarifa kwamba waratibu wa masuala ya udhalilishaji washehia watawezeshwa, ili waweze kukabiliana vyema na mapambano dhidi ya udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Vile vile, Kamati inatoa wito kwa Wizara kuzidisha mashirikiano na wadau mbali mbali ikiwezo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, vyombo vya habari vya serikali na binafsi, Jeshi la Polisi, Mahakama pamoja na jamii kwa ujumla kuhusiana na masuala ya udhalilishaji wa wanawake na watoto katika kuendelea kutoa elimu kuhusiana na ubaya na madhara ya vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika , Kamati inafurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na Wizara ambapo juhudi hizi tumeaza kuziona kwani ni wiki iliyopita tu, Kamati hii kwa kwa kushirikiana na Wizara, Wataalamu kutoka Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Watendaji wa Mahakama na Jeshi la Polisi tulifika katika Vijiji vya Tumbatu na Mkwajuni kuwaelimisha wananchi juu ya vitendo hivi vibaya katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza tena juhudi zinazochukuliwa na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kufanya mikakati ya makusudi ya kuzishughulikia Kesi za Udhalilishaji kwa opereshini Maalum. Tunaomba sana Operesheni hizi ziwe endelevu ili kuvitokomeza kabisa vitendo vya uzalilishaji nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu inazidi kutoa msisitizo kwa Familia zetu zihimize Malezi na maadili mema katika jamii, Taasisi za Kijamii (Shule na Madrasa) zijitahidi kuendelea kutayarisha raia wema. Aidha Dini zetu nazo ziendelee kutilia mkazo Mkazo kukataza maovu, huku tukitekeleza Sheria bora zitakazoweza kuwadhibiti ipasavyo watenda maovu. Pia, Watendaji Haki jinai wawe weledi na waadilifu. Mheshimiwa Spika Tukiyatekeleza hayo Kamati inaamini kwamba tutavikata na kutokomeza kabisa vitendo hivi.

Mheshimiwa Spika, Kamati, imeridhishwa na taarifa ya Wizara kwamba katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara imeweza kutekeleza malengo mbali mbali iliyojipangia yakiwemo ya ununuzi wa magari kwa ajili ya Wazee Sebleni pamoja na Nyumba ya Kulelea Watoto Mazizini, pia kuimarisha huduma za jamii ikiwemo chakula kwa Unguja na Pemba.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na mipango na malengo waliyojipangia kutekeleza, lakini Wizara ijitahidi kuzishughulikia changamoto zilizobakia katika kuimarisha huduma za jamii pamoja na maendeleo ya wanawake ikiwemo kupatiwa Daktari Nyumba ya Kulelea Watoto Mazizini kwa wakati wote, ili kuweza kuwapatia huduma ya afya watoto wetu wanaolelewa katika nyumba ile.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na Wizara kujitahidi kutatua au kupunguza changamoto zinazozikabili idara na taasisi zilizo chini yake, bado kuna changamoto kwa baadhi ya taasisi na idara zilizo chini ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kwa Unguja na Pemba. Baadhi ya changamoto hizo ni hizi zifuatazo:-

(a) Ufinyu wa ofisi za kufanyia kazi
(b) Uhaba wa vitendea kazi
(c) Upungufu wa watendaji au wataalamu katika Idara ya Ajira na Idara ya Usalama na Afya Kazini.

Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Wizara iendelee kuchukua hatua za kukabiliana na changamoto hizo, ili taasisi na idara ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi katika kuleta maendeleo nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu imeridhika na makadirio yaliyopangwa katika programu hii kutokana na kwamba suala la upatikanaji wa ajira ni muhimu sana katika nchi yetu, kwa sababu ya kuongezeka idadi ya watu pamoja na vyanzo kidogo vya ajira. Kwa kweli, uwezo wa Serikali wa kutoa ajira kwa wananchi wote ni mdogo. Kutokana na hali hiyo, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara iliwaunganisha na waajiri vijana kwenda kufanya kazi nchini Qatar, Oman na Jumuiya ya Nchi za Falme za Kiarabu (*U.A.E*) kwenye fani tofauti pamoja na vijana wengine wameajiriwa na taasisi mbali mbali binafsi ndani ya nchi.

Aidha, Kamati inaunga mkono Wizara kwa programu hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo imelenga kufanya mambo mbali mbali yakiwemo kuwezesha jamii kupata fursa za ajira za staha, kuimarisha mashirikiano na wadau na kutoa mafunzo kwa watafuta kazi hasa vijana juu ya kujiajiri na kuajirika. Kamati inaamini kwamba hali hii itaongeza uwelewa kwa watafuta kazi na hasa vijana na kuweza kujiajiri au kuajiriwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Vile vile, Kamati inaisisitiza Wizara kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Sheria ya Kazi kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Ajira Namba 11 ya mwaka 2005 na Sheria ya Mahusiano Kazini Namba 1 ya mwaka 2005, ili waajiri na waajiriwa waweze kufahamu Sheria hizo zinazohusiana na masuala ya Ajira kwa lengo la kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mwisho, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru tena kwa mara nyengine kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati, pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza.
Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii, ili wamewezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliyojipangia kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika,

Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya Wananchi wa Kijitoupele naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Naunga Mkono Hoja.

.....
Mhe. Ali Suleiman Ali (SHIHATA),
Mwenyekiti,
Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.